
www.ippmedia.com

# Alasiri Online

ISSN 0856 Na. 001 Jumamosi Machi 30, 2019 Tanzani 500/- Kenya 50/-





# MARIOO ATAMBA NI WA WOTE

**Na Mary Kadoke**

MTUNZI Marioo amesema siku zote mlango wa utunzi wa ngoma kwa wasanii wengine huwa wazi, na si kama ilivyokaririka kuwa anaofanya nao kazi mara kwa mara ndio mpaka wake.

Amesema hayo alipofanya mazungumzo na Alasiri Online na kuongeza kuwa uchoyo kwake ni mwiko, hufungua mlango na kufanya kikamilifu kazi husika baada ya kuwekeana maridhiano chanya ya pande zote mbili.

"Hakuna msanii mkubwa aliyewahi kunikasirikia kwa sababu nilikataa kumuandikia ngoma," amesema.

"Mtu akija na akitaka nimuandikie kwa makubaliano ambayo tumeyaweka naandika bila shida yoyote," amesema.

Mara nyingi huwa mtunzi wa kazi za Nandy, si huyo tu Gigy pia aliwahi kuandikiwa kazi yake ya Nampa Papa.

Pamoja na utunzi wake ni miongoni mwa wasanii wanaofanya poa kwenye soko la muziki.

Kibao chake cha Dar Kugumu ndicho kilichomuweka mjini mwaka jana kwa shows na trends kwenye redio.

Kwa rekodi zilizozopo, iliwahi kushika Top 20 ya redio ya East Africa.



# BEKA AFUNGUA MOYO

Na Anaeli Mbise

MSANII Beka Flavour ameamua kusema ya moyoni baada ya kueleza Yamoto Band ilimpendelea Dogo Aslay.

Akizungumza na Alasiri Online, amesema baada ya kundi hilo kuvunjika na kuanza kufanya kazi peke yake, hali imekuwa tofauti kwa kuwa nyota imezidi kung'aa na kupata umaarufu zaidi tofauti na huko nyuma.

"Naona nyota yangu inaang'aa na nimekuwa miongoni mwa wasanii maarufu nchini, ninamiliki gari, nyumba na vitu vingine muhimu, vitu ambavyo sikuwa navyo nilipokuwa Yamoto Band," amesema Beka.

Kwa upande wake mwanamuziki Aslay amesema kuwa kipindi wakiwa katika kundi hilo, kila msanii alipewa fursa zao ila ni bahati tu kuwa alifanya vizuri kuliko wengine.

Aidha amemsifia Beka kwa kusema kuwa ni mwanamuziki mzuri mwenye sauti safi na tungo nzuri kwa sababu anafahamu uwezo alionao tangia Yamoto bendi.

Kwa sasa Beka ana ngoma mpya inaitwa Finally, huku Aslay akitamba na kibao kinachokwenda kwa jina la Nyanga'nyang'a.

# KALA JEREMIAH AKERWA

Na Anaeli Mbise

RAPA Kala Jeremiah amefunguka kwamba anakerwa nanyimbo za baadhi ya wasanii zenye mwelekeo wa matusi akisema zinapotosha watoto.

Akizungumza na Alasiri Online, Kala amesema kuna baadhi ya wasanii wanaimba mistari yenye matusi ndani kitu ambacho ni hatari kwa jamii.

"Wasanii wasifikirie pesa tu bali waangalie kile wanachokipeleka kwenye umma kama kina maadili, vinginevyo watakuwa na mchango mkubwa katika kukiharibu kizazi hiki kwa nyimbo zao za ovyo," amesema Kala.

Kala ameongeza kuwa wasanii ni kioo cha jamii na wanatazamwa na kuaminiwa, hivyo wawe makini katika tungo zao badala ya kuangalia pesa zaidi kuliko maadili.

Mwanamuziki huyo wa miondoko ya Hip-hop ametamba na ngoma kali kama Ningekuwa Rais, Usikate Tamaa, Dear God pamoja na Kijana.

# KIKI ZAGAWA WASANII



Na Mary Kadoke

KIKI imeendelea kupata mitazamo tofauti kwa wasanii hasa wa muziki katika kusaka mkate wao wa kila siku.

Muimbaji Barnaba Classic akifanya mazungumzo na Alasiri Online, amesema kwake anamtafsiri mtumia kiki kama mtu asiejiamini.

Akifafanua zaidi kuhusu hilo amesema kufanya kiki ni kutokukomaa kiakili.

"Kufanya kiki ni utoto na kutokutambua thamani yako kama msanii," amesema.

"Baadhi ya wasanii wanapenda kufanya kiki na kwa upande wangu naona ni utoto maana msanii ni kioo cha jamii na wengi walio nyuma wanakutazama kama mfano, hivyo ukizoea kufanya kiki watu watakuchukulia hivyo," amesema.

"Nimelelewa kwenye familia ya maadili si tu kwenye familia, mpaka muziki, kuna watu wananipenda hivyo siwezi kubomoa thamani yangu kwa stori za muda mfupi," amesisitiza.

Si Barnaba tu ambaye hakubaliani na kiki katika tasnia ya Bongo Fleva, akifanya mazungumzo na Alasiri Online, Kayumba Assosie hivi karibuni, aliweka msimamo wa kutokukubaliana na kiki kwani juhudi zake na muziki bomba anaojitahidi kufanya ndio silaha zake za ushindi.

Pamoja na misimamo hiyo ya Barnaba na Kayumba, kiki huonekana kuwabariki baadhi ya wasanii, hivyo kuamua kuitumia baada ya kuona kuwa itawanufaisha katika muziki wao.

Hamisa Mobetto ni muumini mzuri wa kiki, mwishoni mwaka jana kabla ya kuzindua kibao chake cha Tunaendana, zilizuka habari za Hamisa kumpata mrithi wa mzazi mwenzake Diamond Platnumz.

Hiyo kufanya watu kuwafuatilia kwa ukaribu zaidi kwenye mitandao ya kijamii mahaba yao motomoto yaliyoonekana kupitia ukurasa wa Instagram wa @ Hamisamobetto.

Hata hivyo, baadaye ilikuja kugundulika kuwa kibao chake kipya na aliyepamba kibao hicho 'Video King' alihusika mpenzi wake.

Mpaka sasa wimbo huo una watazamaji milioni moja katika mtandao wa YouTube.



# REMMY ANAPENDA UBOSI

Na Mary Kadoke

'MTU mwenye wadhifa' ndio uhusika unaomkonga nyoyo muigizaji Rammy Galis.

Akifanya mazungumzo na Alasiri Online amesema hufanikiwa kufikisha ujumbe vizuri katika nafasi hiyo kwani ndiyo maisha anayokumbana nayo kila siku.

"Napenda kuigiza scene zinazoonesha maisha fulani hivi ya wadhifa, maana ni maisha ambayo nayaishi," amesema.

"Scene za umaskini ni ngumu sana kwangu kwani ni maisha ambayo sijayapitia kihivyo, inanichukua muda kuyaigiza," ameongeza.

Tofauti na kuigiza hupata dili mbalimbali za kutangaza bidhaa au maeneo ya biashara.

Kwa mfano mwaka jana alibahatika kuwa balozi wa City Mall Cinema Hall. Filamu iliyomtambulisha zaidi ni Vocha na Zakayo.



# Nyoshi: Viwaro vinapandisha chati

Na Mary Kadoke

RAIS wa bendi ya Bogos Musica Nyoshi El Saadat ameeleza kuwa mara nyingine muonekano wa msanii ni kitu cha kuzingatia ili kuendelea kuvutia mashabiki kupenda kazi yako.

Ameyasema hayo alipofanya mazungumzo na Alasiri Online akisisitiza kuwa, wasanii hupoteza muda kutafuta mchawi wa kukwama kwao pasipo kutambua kuwa muonekano ni silaha mbadala wa mafanikio yao.

"Unaweza kuwa muimbaji mzuri, unacheza vizuri, lakini kama hupendezi huwezi kupendeza huwezi kuwavutia mashabiki," amesema.

"Utakaa unashangaa wenzako wanafanya vizuri huku wewe unakwama," amesema.

"Unapaswa kupendeza mpaka shabiki akikuona anajiuliza huyu kwa alivyopendeza nimtunze shilingi ngapi?" ameuliza.